

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

03/06/2019

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA ATIMIZA AHADI YA KUWASHIKA MKONO WACHEZAJI WA SIMBA, AWAKABIDHI KITITA CHA MILIONI 24.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda leo amewakabidhi wachezaji wa Simba kitita cha Shilingi Milioni 24 kama sehemu ya zawadi na hamasa kufuatia Timu hiyo kuchukuwa ubingwa wa Ligi kuu Tanzania bara na kuingia katika robo fainali ya Klabu bingwa Afrika.

RC Makonda amewataka wachezaji hao kutumia fedha hizo kuanzisha miradi ya maendeleo itakayowasaidia kujipatia kipato pindi watakapostaafu mpira huku akiwataka kutumia umaarufu na Brand zao kujiingizia kutengeneza kipato.

Aidha RC Makonda amesema katika mgawanyo wa fedha hizo Golikipa wa Simba Aish Manula amepokea kiasi cha Shilingi Milioni10, Wachezaji tisa Milioni 1 kila mmoja, Mchezaji bora wa kike wa Simba Queen Milioni 2 na Msemaji wa Simba Haji Manara ambae amepatiwa Milioni 3 kama sehemu ya kutambua mchango wake kwenye uhamasishaji wa mashabiki kujaa uwanjani.

Pamoja na hayo RC Makonda amewaasa wachezaji kuongeza morali ya uchezaji ili waendeleo kunyakua ubingwa na kushika nafasi za juu katika ligi za kimataifa.

Hata hivyo RC Makonda amewataka wachezaji kuchukulia michezo kama pesa, uchumi, Amani na biashara inayoweza kuwafanya hao binafsi wanufaike kiuchumi na kulipatia taifa mapato ya kutosha kupitia mapato yanayoenda kwenye Manispaa.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM